HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

TOLEO LA 004 | SEPTEMBA 2022 | HALIUZWI

# Jarida la TEMEKE YETU

FAHAMU ZAIDI



# TEMEKE YABORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU

"Jitihada hizi zimeongeza idadi kubwa ya miundombinu na samani katika sekta ya Elimu ya Msingi na kufanikiwa kuongeza ufaulu hadi kufikia asilimia 94.8% mwaka 2021-2022".
- Ndg. Elihuruma Mabelya

HABARI KAMILI UK. 2



## TUNATAKA KUACHA ALAMA NZURI

Manispaa ya Temeke inahitaji kuwa na vitega uchumi vyake ambavyo vitakuwa chanzo cha uhakika cha mapato...

HABARI KAMILI UK. 3

MHARIRI MKUU
**FRANCISCA MSELEMU**

WAHARIRI WASAIDIZI
**SHARUA MPANDA**
**SWEETBETTER NJIGE**
**NASSORO RASHID**

WAPIGA PICHA
**MATHEW JONAS**
**VICTOR DEOGRATIUS**

MSANIFU WA JARIDA
**MICHOLAX HARRY MUSSA**

JARIDA HILI HUTOLEWA NA;
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
S.L.P 46343 Temeke, DSM.
SIMU: +255 22-2928132
NUKUSHI: +255 22-2928137
BARUA PEPE: temeke@temekemc.go.tz



# TEMEKE YABORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU.



Na **Jackson Wilson TMC Habari.**

Wakati Tanganyika inapata uhuru baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema kuna maadui watatu ambao ni ujinga,umaskini na maradhi, Katika kupambana na ujinga elimu ni silaha tosha ya kuhakikisha jamii inajikomboa kwa kujenga miundombinu rafiki ya elimu. Halmashauri ya Manisipaa ya Temeke imezidi kuonesha mapambano kwa adui huyo kwa kuboresha miundombinu ya elimu.

Akizungumza na Waandishi wa Habari katika ukumbi wa Iddi Nyundo, Mkurugenzi wa Manispaa hii ndugu Elihuruma Mabelya amesema Manispaa imezidi kuboresha na kuweka mazingira rafiki ya utoaji wa elimu.

"Kupitia idara ya Elimu Sekondari Manispaa imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali yenye thamani ya shilingi za Kitanzania Bilioni 4.8 ambazo zimetumika katika ujenzi wa vyumba vya darasa 175,bweni 1,bwalo 1,matundu ya vyoo 90, maabara 12, shule mpya 1 ambayo ni Shule ya Sekondari ya Dovya pamoja na ununuzi wa madawati ( viti na meza) 9584 .

Katika idara ya Elimu Msingi Manispaa imefanikiwa kujenga Madarasa 1598, matundu ya vyoo 1797,ununuzi wa madawati 37, miundombinu yote hii imetumia shillingi za Kitanzania billioni 1.4.

"Jitihada hizi zimeongeza idadi kubwa ya miundombinu na samani atika sekta ya Elimu ya Msingi na kufanikiwa kuongeza ufaulu hadi kufikia asilimia 94.8% mwaka 2021-2022".

Haya ni mafanikio makubwa katika sekta ya elimu hasa ukizingatia idadi kubwa ya wanafunzi, hivyo Manisipaa imeweza na inaendelea kupambana na adui huyu ambaye Baba wa Taifa aliagiza tupambane dhidi yake.

# TUNATAKA KUACHA ALAMA NZURI: NAIBU MEYA

Na **Sharua Mpanda**
**TMC Habari.**

Naibu Meya wa manispaa ya Temeke Mhe. Arnold Peter leo Septemba 29,2022 ameendesha kikao cha baraza la Madiwani kilichojadili hesabu za mwisho za Manispaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30,Juni 2022.

Akizungumza katika kikao hicho kilichohudhuriwa pia na wakuu wa idara na vitengo wa Manispaa hiyo, Mhe. Peter amesema wao kama wawakilishi wa Wananchi wanapaswa kuacha "alama" katika utumishi wao.

Naibu Meya huyo ambaye kwenye kikao hicho alikuwa Mwenyekiti, amesema manispaa ya Temeke inahitaji kuwa na vitega uchumi vyake ambavyo vitakuwa chanzo cha uhakika cha mapato ya Manispaa hiyo.

Awali akichangia hoja katika kikao hicho, diwani wa kata ya Kilungule Mhe.Saidi Fella alitaka kujua katika mgawanyo wa mali mara baada ya kugawanywa kwa wilaya ya Temeke na Kigamboni, manispaa ya Temeke ilipata zipi.



"Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata kigugumizi kuelewa,mwanzoni kabla ya kugawa wilaya ya Kigamboni na Temeke, lile jengo la Mkuki(Mkuki house) lilikuwa huku kwetu,nataka kufahamu sisi sasa hivi tumebaki na nini?".Alisema Mhe.Fella.

Mara baada ya majadiliano hayo Madiwani hao walipitisha hoja zote huku kikao hicho pia kikitoka na maazimio mawili mojawapo likiwa ni kuandaa kikao maalum cha kujadili masuala ya uwekezaji.

***"Niwapongeze kwa maandalizi ya ripoti hii nzuri ambayo kwa matarajio mazuri na hii inaonesha ni jinsi gani mmejiandaa niwashukuru pia kwa uwasilishaji mzuri".***

*Mhe.Arnold Peter*
*Naibu Meya - Manispaa ya Temeke*

# DC JOKATE ATOA MAAGIZO MATATU.



Na **Sharua Mpanda**
**TMC Habari.**

Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Jokate Mwegelo Agosti 27,2022 ameshiriki zoezi maalum la usafi wa mazingira katika kata ya Chamazi na kutoa maagizo matatu.

Agizo la kwanza ambalo Mhe.Jokate ametoa ni kwa makarani wa Sensa ambapo amewataka makarani hao kufanya kazi hiyo kwa uadilifu na kuhakikisha kila Mwananchi anafikiwa na kuhesabiwa.

'Nataka kuona Chamazi na Temeke kwa ujumla tunafanya vizuri,zoezi hili ni muhimu na nyeti sana.Fanyeni kazi hii kwa uadilifu."Alisema



Pia alitumia nafasi hiyo kuwataka wafanyabiashara ndogondogo(Machinga), kuondoka maeneo ambayo sio rasmi kwa biashara.

Mhe.Jokate ametoa agizo kuwa kuanzia Septemba 05,2022 ni marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kuwataka Wananchi kutoa ushirikiano pindi wanapoona matumizi na utengenezaji wa mifuko hiyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amewapongeza wakazi wa kata ya Chamazi kwa namna walivyojitokeza katika zoezi la usafi na kuwataka waende lee kudumisha usafi katika maeneo yao.

Zoezi hilo la usafi ni muendelezo wa kampeni maalumu ya usafi kwa mkoa wa Dar es salaam,mwanzilishi wake ni Mkuu wa mkoa huu Mhe.Amos Makalla ambapo alitoa maelekezo kuwa Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi itakuwa ni siku ya usafi.

# TUMEKUJA KUJIFUNZA TEMEKE - MADIWANI MVOMERO.




Na **Sharua Mpanda**
**TMC Habari.**

Maonesho ya wakulima maarufu Nanenane yaliyofanyika kuanzia Agosti Mosi, 2022 mkoani Morogoro yamekuwa na mafanikio makubwa kutokana na muitkio mkubwa wa wananchi waliojitokeza katika Maonesho hayo. Banda la Halmashauri ya manispaa ya Temeke limeendelea kuwa kivutio katika Maonesho hayo ambapo Agosti 6,2022 lilitembelewa na madiwani wa halmashauri ya wilaya ya Mvomero wakiongozwa na makamu mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mhe.Christopher Maarifa ambaye pia ni diwani wa kata ya Mangae wilayani Mvomero.

Wakiwa ndani ya banda hilo,madiwani hao wapatao 40 walipata fursa ya kujionea na kujifunza shughuli mbalimbali zinazofanywa na wajasiriamali na wakulima wanaotoka wilayani temeke. "Nimekuwa nikisikia tu sifa kutoka kwa watu huko kuhusu mambo yanayofanywa hapa Temeke na mimi nikashauri tuje kupita hapa na kujifunza jinsi gani ya mikopo ile ya asilimia 10,na nimeona vitu vingine ambavyo sijawahi kuviona kama aina hii ya samaki mkunga".Aliongeza Mhe.Christopher.

Naye Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira wa Halmashauri hiyo Mhe.Jailos John Msigwa amesema kuwa wameweza kujifunza mambo mengi kupitia ziara yao hiyo na wataenda kufanyia kazi yale waliyojifunza.

Ziara hiyo ya madiwani ni muendelezo wa wageni mbalimbali wanoendelea kutembelea banda la manispaa ya temeke lililopo ndani ya viwanja vya Mwl.Nyerere maarufu kama Nanenane mkoani Morogoro ambapo elimu na mafunzo mbalimbali yanaendelea kutolewa juu ya kilimo bora,ufugaji,uvuvi na ujasiriamali ili kuhakikisha kilimo kinakuwa cha kibiashara ifikapo mwaka 2030.

# MKURUGENZI MABELYA AMTEMBELEA BALOZI LUMBANGA


Na **Sweetbetter Njige - TMC Habari.**

Septemba 20,2022 mkurugenzi wa manispaa ya Temeke Ndugu Elihuruma Mabelya amemtembelea nyumbani kwake mheshimiwa balozi mstaafu Marten Lumbanga kwa ajili ya kumjulia hali na kuzungumza naye juu ya masuala mbalimbali ya uongozi na serikali kwa ujumla.

Mkurugenzi Mabelya amempongeza mzee Lumbanga kwa kuitumikia serikali ya Tanzania kwa upendo na uzalendo na kuendelea kuwa mshauri kwa viongozi vijana.

Balozi Lumbanga alihudumu kama katibu mkuu kiongozi kuanzia mwaka 1995-2006, balozi wa Tanzania nchini Uswisi kuanzia mwaka 2006-2012 na mwenyekiti wa bodi ya PPRA kuanzia mwaka 2012 mpaka Septemba 2022.

"Leo tumekuja kukutembelea nyumbani kwako kwakua unastahili heshima hiyo, Serikali inakuthamini na haiwezi kukutupa kwakua umeitumikia kwa auaminifu mkubwa, kwa maagizo ya mhe. mkuu wa mkoa Amos Makalla na ushirikiano baina ya ofisi ya mkuu wa wilaya mhe. Jokate Mwegelo na manispaa ya Temeke tutaendelea kuwa karibu na wewe kwaajili ya maendeleo ya Serikali yetu".





# MKURUGENZI TEMEKE AELEZA MAFANIKIO.



Na **Sharua Mpanda TMC Habari.**

Mkurugenzi wa halmashauri ya manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amekutana na wandishi wa Habari leo Septemba 29,2022 kueleza mafanikio ambayo yamepatikana kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22.

Mkurugenzi Mabelya ameeleza kuwa katika kipindi hicho manispaa ya Temeke ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 37 lakini ikakusanya bilioni 39 sawa na asilimia 106%.

Kwa upande wa elimu sekondari,Manispaa imeweza kutekeleza miradi mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 4.8 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa 175,bweni 1,bwalo 1,matundu ya vyoo 90,maabara 12,shule mpya moja na miundombinu ya maji.

"Mafanikio haya yametokana na ushirikiano mkubwa wa Baraza la madiwani likiongozwa na Mstahiki meya Mtinika,wamekuwa wakituongoza pale walipoona tunakosea, tunawashukuru sana".Alisema

Pamoja na kuainisha mafanikio katika sekta zote ikiwemo afya,maendeleo ya jamii, ujenzi nk,Mkurugenzi amesisitiza juhudi na uwajibikaji katika kazi ili kuendelea kuhudumia Wananchi kwa kuwa maendeleo hayana kikomo.

Aidha amewashukuru Wananchi kwa kuelewa umuhimu wa kulipa kodi na tozo mbalimbali hali inayochangia kuongezeka kwa mapato ya ndani ambayo yanawezesha kujenga miundombinu.

Pia amemshukuru mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha katika Manispaa hii ambapo amesema katika kuboresha sekta ya afya, serikali Kuu imetoa kiasi cha shilingi bilioni 2 kufanya upanuzi wa hospitali ya Mbagala Rangitatu.

Manispaa ya Temeke imepanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 43 kwa mwaka wa fedha 2022/23 ,ili kufikia lengo hilo,Mkurugenzi amewasihi Wananchi kuendele kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kulipa kodi.

# SERIKALI YATANGAZA OPERESHENI MAALUM KUTUNZA MTO KIZINGA

Na **Sharua Mpanda**
**TMC Habari.**

Katika kuhakikisha rasilimali za vyanzo vya maji zinatunzwa Serikali imetangaza zoezi maalum la kubaini wachafuzi wa chanzo cha maji cha mto Mzinga. Akitoa taarifa ya zoezi hilo katika kikao cha watendaji wa Kata na wenyeviti wa Serikali za mitaa,Afisa maendeleo wa jamii kutoka Wizara ya maji Bi.Flora Muro amesema kuwa mto Mzinga ni chanzo kikuu cha maji ambacho kinapaswa kutunzwa.

"Tumekubaliana kuwa siku ya Jumatatu na Jumanne tutaanza kazi ya kuelimisha wananchi kwa Kata tatu na Mitaa yake na kuweka mabango ya makatazo kwenye mita 60 ili watu wasiendelee na shughuli zozote katika maeneo hayo". Alisema Bi.Muro

Kikao hicho kilichojumuisha watendaji kata wa kata za Chamazi,Kilungule na Buza pamoja na wenyeviti wa Mitaa kutoka katika Kata hizo, kinafuatia uwepo wa shughuli zinazofanywa na wananchi karibu na Mto huo ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu na uchafuzi chanzo hicho kikuu cha upatikanaji wa maji katika mkoa wa Dar es salaam.

Naye mtendaji wa kata ya Chamazi Bi.Dafrosa Lyimo amesema wamepokea maelekezo hayo na watashirikiana na wataalamu hao kutoka Bodi ya maji bonde la Wami-Ruvu kidakio cha Pwani ili kuweza kutunza mazingira kwa kizazi cha sasa na baadae. Mto Kizinga ndio chanzo kikuu kinachotegemewa na Mamlaka ya Maji Safi Dar es salaam (DAWASA) kuweza kuhudumia Mkoa huo wenye idadi kubwa ya watu hapa Nchini.

## TIMU YA MADAKTARI BINGWA YAPIGA KAMBI SIKU TATU TEMEKE KUTOA HUDUMA ZA AFYA BURE

Uongozi wa hospitali ya rufaa ya mkoa wa Temeke kwa kushirikiana na ofisi ya mkurugenzi wa Manispaa hii ,uliandaa zoezi la utoaji wa huduma za afya bure kuanzia Septemba 9 hadi 12,2022.

Akizungumza na waandishi wa Habari Septemba 5,2022 mganga mfawidhi wa hospitali ya rufaa ya mkoa wa Temeke Dkt. Joseph Kimaro amesema zoezi hilo litaendeshwa na timu ya madaktari Bingwa ambapo kutakuwa na huduma za upimaji afya na matibabu bila malipo.

"Hii ni fursa kwa wananchi wa Temeke kupata huduma za Kibingwa,na lengo la zoezi hilo ni kuhakikisha huduma hizo zinawafikia Wananchi wengi kwa kadri inavyowezekana"Alisema Dkt Kimaro. Awali mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya zoezi hilo linalojulikana kama "Temeke Afya Check" na daktari bingwa wa kinywa na meno Dkt Twisibilega Mwakasungule alisema huduma zitakazotolewa ni pamoja na magonjwa ya Wanawake na Uzazi,magonjwa ya Watoto na mengine mengi.

Amesema kuwa madaktari Bingwa hao watatoa huduma na ushauri wa Kitaalam bure na kuwataka Wananchi kujitokeza kwa wingi katika zoezi hilo kupata huduma hizo.

Zoezi hilo ambalo lilihudumia zaidi ya watu 5,000 lilifadhiliwa na wadau mbalimbali wa afya wakiwemo MDH, Haidery Plaza, NMB, CRDB, CCBRT, Shamshu Pharmacy,Serengeti, NBC na wengine ambapo lilianza rasmi Septemba 9 hadi 12 ,2022 kuanzia saa 2:30 asubuhi mpaka saa 09:30 alasiri.

# MAMA WA MAPACHA WANNE APEWA MSAADA WA PIKIPIKI




Na **Jackson Wilson TMC Habari.** Mkuu wa wilaya ya Temeke Mheshimiwa Jokate Mwegelo leo Septemba 29, 2022 amemkabidhi pikipiki Bi Fatuma Mtopela ambaye alijifungua watoto wanne.

Mhe Jokate amesema mama huyo ambaye alijifungua mapacha hao mwezi Februari mwaka huu amekuwa akipata changamoto za kuhudumia watoto hao, hivyo Ofisi yake imeamua kumsaidia pikipiki ili iweze kumpatia kiasi cha fedha kwa ajili ya mahitaji ya watoto.

"Tumeona kuliko kila siku kuja ofisini kumchangia maziwa na vitu vidogovidogo, ni bora kumuwezeshe kiuchumi, aweze kujitegemea na kuweza kuwahudumia watoto wake".Alisema Mhe.Jokate

Pia Mhe.Jokate ametoa wito kwa Wananchi na wadau mbalimbali kujitokeza kumsaidia mama huyo ambaye ana jumla ya watoto saba.

Kwa upande wake Bi.Fatuma amemshukuru Mkuu huyo wa wilaya kwa kupatia pikipiki hiyo ambayo itakuwa msaada mkubwa kwake. Mama huyo mwenye watoto saba amesema watoto wake wanahitaji maziwa litambili na nusu kila siku na mahitaji mengine ambapo ameomba Watanzania wamsaidie kwa kutumia namba ya simu 0788508645.



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI






# MANISPAA YA TEMEKE YAKABIDHIWA VIFAA TIBA




Na **Sweetbetter Njige, TMC Habari.** Katika kuadhimisha siku ya majeshi ya Afrika Mashariki, Jeshi la Wananchi wa Tanzania(JWTZ) limetoa msaad wa vifaa tiba na madawa pamoja na huduma za matibabu bure katika hospitali ya Mbagala Rangitatu.

Akizungumza leo Agosti 29,2022 katika hafla fupi ya makabidhiano ya vifaa hivyo na kufungua rasmi utoaji wa huduma ya matibabu bure katika Hospitali hiyo, Meja Jenerali Gabriel Mhidze amesema pamoja na huduma hiyo ya afya ambayo itatolewa kwa siku tatu kuanzia leo Agosti 29 hadi Agosti 31 mwaka huu, pia watatoa misaada katika vituo vya watoto yatima na vinavyohudumia wazee.

"Lengo kubwa la wiki ya majeshi ya Afrika Mashariki ni kuyaleta majeshi yetu karibu ili kuyaunganisha na kuyafanya kuwa karibu na Wananchi ili kufikia lengo la Afrika Mashariki na kuondoa fikra tofauti zilizopo".Alisema Meja Jenerali Mhidze

Naye mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Mhe. Abdallah Mtinika ameushukuru uongozi wa Jeshi hilo kwa kuichagua hospitali ya Mbagala Rangitatu kuleta misaada hiyo, pamoja na huduma za afya ambapo ametoa wito kwa Wananchi kujitokeza kwa wingi katika siku hizo za matibabu bila malipo.

Mkazi wa Mbagala Bi.Sofia Kilango amemshukuru mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha huduma za afya hasa za wakina Mama na Watoto.

Septemba 01,2022 Tanzania itaadhimisha siku ya majeshi, ikiwa ni miaka 58 toka kuanzishwa kwa JWTZ mwaka 1964.Kuelekea siku hiyo, madaktari wa jeshi hilo wanatoa huduma za kibingwa katika vituo mbalimbali vya afya Nchini sambamba na kutoa misaada ya vifaa tiba na madawa katika vituo vya Afya pamoja na misaada ya kijamii katika vituo vya kulelea watoto yatima na makao ya wazee wasiojiweza.

# TEMEKE IMEPIGA HATUA UDHIBITI WA MAPATO-NAIBU MEYA ZNZ



Na **Nassoro Rashid**
**TMC Habari.**

Imeelezwa kuwa manispaa ya Temeke ni moja kati ya manispaa zinazofanya vizuri katika udhibiti wa mapato yanayotokana na malipo ya maegesho kutokana na mfumo unaotumika.

Hayo yameelezwa na Naibu meya wa manispaa ya Mjini Zanzibar mheshimiwa Khadija Haji alipokuwa katika ziara ya kimafunzo ya siku moja wilayani Temeke kujifunza jinsi manispaa ya Temeke inavyokusanya mapato Agosti 12,2022.

Akiwa ameambatana na baadhi ya waheshimiwa madiwani na wataalam kutoka Zanzibar,waliweza kutembelea maeneo ya maegesho ya magari eneo la Quality group barabara ya Nyerere ambapo walipata maelezo jinsi ya kutumia mfumo wa ukusanyaji wa mapato hayo.

"Tumeamua kuja kujifunza Temeke kwa sababu wenzetu wamepiga hatua kubwa sana katika kudhibiti upoteaji holela wa mapato ambapo tunaamini endapo tutafanya hivi basi tutakusanya mapato zaidi".Alisema Mhe.Khadija

Katika ziara hiyo pia Viongozi hao walitembelea ofisi za TARURA halmashauri ya Jiji ambapo waliweza kupata nafasi ya kuona mfumo mzima wa ukusanyaji wa mapato hayo kupitia kwa wahasibu wa halmashauri ya jiji la Dar es salaam.

Ziara hii ni muendelezo wa ziara nyingine za mafunzo zinazofanywa na baadhi ya halmashauri hapa nchini kuja kujifunza namna manispaa ya Temeke inavyofanya kazi katika nyanja tofauti.

# BILIONI 2 ZATOLEWA KUFANYA UPANUZI HOSPITALI YA MBAGALA RANGI TATU.




*Ujenzi wa jengo hilo la ghorofa sita utakuwa ni muarobaini wa kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali inayohudumia wakazi wengi wa Mbagala na wilaya za jirani na hata baadhi ya wakazi kutoka mkoa wa Pwani kama Mkuranga.*

Na **Sharua Mpanda**
**TMC Habari.**

Suala la msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya Mbagala Rangi tatu linaweza kubaki historia katika siku zijazo baada ya Serikali ya awamu ya sita chini Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kutoa kiasi cha shilingi bilioni 2 kutekeleza upanuzi wa Hospitali hiyo.

Akiongea na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Mei 26, 2022 katika viwanja vya Zakhem Mbagala, diwani wa kata ya Mbagala kuu Mhe. Mahanya Juma Mahanya, amesema kuwa wana kila sababu kumshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia kiasi hicho cha fedha ambacho tayari kimeshaingia kwenye akaunti ya hospitali.

"Ninayo furaha kuona Serikali yetu sikivu ya awamu ya 6 inayoongozwa na mama yetu Samia Suluhu Hassan, inavyoweza kusikiliza na kutekeleza kwa vitendo Ilani ya chama chetu; Chama Cha Mapinduzi". Alisema Mhe. Mahanya.

Akisoma taarifa hiyo kwa mgeni rasmi, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo Dkt Ally Mussa,amesema hospitali ya Mbagala Rangi tatu kwa sasa inahudumia wagonjwa takribani elfu moja mpaka elfu moja mia mbili kwa siku huku idadi ya wamama wanaojifungua kwa siku ikifika 40 hali ambayo inaonesha uhitaji wa majengo ya kutosha.

Mjumbe wa bodi ya afya hospitalini hapo Bw.Ernest Nyambo amedai kuwa ujenzi wa jengo hilo utapunguza msongamano wa wagonjwa na rufaa zinazotolewa kwenda katika hospitali za Mikoa na hata ya Taifa Muhimbili.

# TEMEKE YATOA BILIONI 1.8 KUWAKOPESHA VIJANA,WANAWAKE NA WENYE ULEMAVU



Na **Sharua Mpanda**
**TMC Habari.**

Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke mheshimiwa Abdallah Mtinika amesema kuwa Manispaa hiyo hapo awali ilikuwa ikitoa mikopo lakini Wananchi wengi hawakuwa wanapata taarifa hali iliyochangia malalamiko kwa baadhi yao.

Mstahiki Meya Mtinika ameyasema hayo alipokuwa akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi hundi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya mikopo kwa vikundi 167 vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu,iliyofanyika katika viwanja vya shule ya sekondari Kibasila Juni 28,2022.

”Niseme tu kwa kifupi mheshimiwa mkuu wa Mkoa,linalotendeka hapa leo ni wazo lako.Temeke tumekuwa tukitoa mikopo ya asilimia 10 lakini tumekuwa tukitoa kimya-kimya , nikushukuru wewe, ni mkuu wa Mkoa lakini pia umekuwa ni Mwalimu, niwaombe ndugu zangu hii mikopo tukiipata tusiache kulipa”. Aliongeza Mhe. Mtinika.

Akisoma taarifa ya utoaji mikopo kwa mkuu wa Mkoa,mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya alisema kuwa Manispaa imekuwa ikitekeleza sheria ya fedha ya serikali za Mitaa ya mwaka 2019 inayoitaka kila Halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kukopesha Vijana,Wanawake na watu wenye Ulemavu ili kuboresha maisha yao.

Kutolewa kwa mikopo hiyo hadharani ni ushauri uliotolewa na mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mhe. Amos Makalla ambapo alipendekeza mikopo itolewe kwa uwazi ili kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa jamii kuwa mikopo hiyo hutolewa kwa baadhi ya watu,sambamba na kuondoa mianya ya rushwa.

# RAIS AMESHATOA FEDHA,MKANDARASI SIMAMIA KAZI IKAMILIKE NDANI YA MUDA" WAZIRI BASHUNGWA





Na **Sweetbetter Njige TMC Habari.**

Waziri wa nchi ofisi ya Rais – TAMISEMI mheshimiwa Innocent Bashungwa amemuelekeza mkandarasi mshauri 'Group Six International Limited' kuhakikisha kuwa kufikia Septemba 30,2022 mradi wa ujenzi wa barabara ya Nzasa Kilungule - Buza uwe umekamilika .

Waziri Bashungwa ametoa maelekezo hayo leo Julai 08,2022 wakati wa ziara yake ya utekelezaji wa ilani ,aliyoifanya katika halmashauri ya manispaa ya Temeke ambapo amekagua barabara ya Nzasa Kilungule Buza ,ujenzi wa daraja pamoja na kituo cha mabasi Buza.

Mara baada ya kukagua barabara hiyo mheshimiwa Bashungwa alikuwa na haya ya kusema "Waheshimiwa wabunge wa Temeke wamekuwa wakifuatilia kwa nguvu kubwa sana juu ya utekelezaji wa barabara hii ambayo tunaitembelea, barabara ya Nzasa Kilungule Buza.

Nimshukuru sana Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan na serikali anayoiongoza ya awamu ya Sita alitoa bilioni 21.5 kwa ajili ya kutatua kero ya wananchi wa Temeke. Na mimi nimefika kwa niaba ya Mhe. Rais kuona bilioni 21.5 ambayo alituwezesha kupitia ofisi ya Rais – TAMISEMI, TARURA kwenye miradi ya DMDP , utekelezaji wa hii barabara unavyokwenda.

Nikupongeze sana pia Mhe. mkuu wa Wilaya kwa namna ambavyo umesimamia jambo hili, lakini kwa ujumla unavyosimamia utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi ndani ya wilaya ya Temeke,lakini vile vile Mkurugenzi kwa namna ambavyo unamsaidia mkuu wa Wilaya katika kusimamia yale ambayo yanahusu Halmashauri"

Naye mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe. Jokate Mwegelo amemhakikishia Mhe. Bashungwa kuwa shughuli za serikali wilayani humu zinasimamiwa vizuri."Mhe. sisi kazi yetu kubwa ni kuhakikisha tunasimamia utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi,kusimamia fedha ambazo Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan analeta kwa ajili ya kuwakomboa Wananchi."Alisisitiza Mhe. Jokate.

# WAKIWEZESHWA WANAWEZA" - MHE. DOROTH KILAVE





Na **Sweetbetter Njige**
**TMC Habari.**

Mbunge wa Temeke Mhe. Doroth Kilave leo Julai 12, 2022 amekabidhi msaada wa vifaa vya kusomea kwa wanafunzi wenye ulemavu wa akili na usonji vilivyotolewa na taasisi ya Diamonds in the Sky Foundation katika shule ya msingi Yombo Dovya iliyopo kata ya Makangarawe wilayani Temeke.

Akizungumza katika hafla hiyo Mhe. Kilave ameishukuru taasisi hiyo kwa mchango wao huo pamoja na walimu huku akiwaomba kuendelea na moyo huo wa kuwasaidia watoto hao kwani ni sehemu ya kusaidia sekta ya elimu na kuwakuza vyema katika elimu yao.

"Nimeambiwa mna wanafunzi 66 lakini mna madarasa mawili ambalo moja mnatumia chumba cha kulia chakula na moja mnafundishia, kwahyo n iwaombe sana nalichukua jukumu hili kama mwakilishi wenu wa wananchi tutaweza kufanya chochote kuongeza darasa moja ili mupate chumba cha kulia na watoto wakae kwenye madarasa mawili" alisema Mhe. Kilave

Pia Mhe. Kilave ametoa wito kwa wazazi, walezi ambao wanatabia ya kuwaficha watoto wenye ulemavu kwani wanawanyima haki zao huku akisisitiza kuwa katika zoezi la sensa linalotarajiwa kufanyika Agosti 23, 2022 wanahaki ya kuhesabiwa hivyo wazazi wawatoe na wawawezeshe kwa kuwapa elimu ili ije kuwasaidia baadae.

Naye kaimu afisa tarafa wa Chang'ombe ndugu Hija Kiteleka akitoa salamu za Mkuu wa wilaya wa Temeke Mhe. Jokate Mwegelo amewashukuru walimu kwa jitihada kubwa wanazozionesha katika kuwafundisha wanafunzi hao wenye ulemavu na kutoa wito kwa wadau wengine wa maendeleo kuwashika mkono wanafunzi wa makundi maalumu ili kuwawezesha na kuwajengea ufahamu kupitia elimu.

Sambamba na hayo naye mkurugenzi wa taasisi ya Diamonds in the Sky Foundation Bi. Jacqueline Lussa kupitia kauli mbiu yao "mlete mtoto, usimfiche" amesema wamependelea kusapoti watoto hao wenye ulemavu katika shule hiyo baada ya kuona ina uhitaji mkubwa sana kulinganisha na shule zingine 4 ambazo wamezitembelea pia ameomba kwa wale walezi, wazazi wanaoficha kuwatoa watoto hao ili waendelee kuwasaidia kwani wana haki na wakipewa nafasi wanaweza wakafika mbali sana.

# MSTAHIKI MEYA AIPONGEZA AZAM FC KWA KUIBUA VIPAJI VYA WATOTO




Na **Nassoro Rashid**
**TMC Habari.**

Uongozi wa kampuni ya SSB Group unaomiliki timu ya soka ya Azam Football Club umepewa pongezi kwa kuthamini na kuendeleza vipaji vya watoto katika soka.

Pongezi hizo zimetolewa na Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke mheshimiwa Abdallah Mtinika Julai 17, 2022 katika siku maalum ya watoto (Azam Child Day) iliyoandaliwa na Timu hiyo katika uwanja wa Azam Complex Chamazi Mbagala.

Akizungumza na wazazi pamoja na watoto uwanjani hapo Mstahiki Meya aliwapongeza viongozi wa Azam Fc na uongozi mzima wa SSB Group kwa kuwekeza kwenye soka la watoto na pia aliwashukuru kwa kujitolea kwao kuwasaidia watoto kufikia malengo yao fursa ambayo watoto walikuwa wanaikosa.

"Fursa hii hapo mwanzoni watoto walikuwa hawaipati ila kwa sasa wanaipata Azam bila malipo yoyote, kikubwa ni mzazi kumruhusu mtoto wake akimuona ana kipaji". Alisema Mtinika

Katika hatua nyingine Meya Mtinika aliwahimiza wananchi wa Temeke kuipenda na kuishabikia timu ya Azam Fc kwa kuwa ni walezi wa watoto wao na pia ni timu iliyopo ndani ya manispaa ya Temeke.

Pia alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha wazazi na wananchi kwa ujumla kushiriki zoezi la Sensa ya watu na makazi litalofanyika nchi nzima Agosti 23, 2022 ili kuunga mkono juhudi za Serikali za kuleta huduma kwa jamii.

# HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA TEMEKE KUANZA KUTOA HUDUMA ZA CT-SCAN.



Na **Nassoro Rashid**
**TMC Habari.**

Katika kuboresha huduma za afya nchini ,Serikali inatarajia kununua mashine ya "CT-SCAN" katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke ili kuwezesha Wananchi kupata huduma hiyo kwa urahisi.

Hayo yameelezwa na mganga mfawidhi wa Hospitali hiyo Dkt. Joseph Kimaro wakati wa uzinduzi wa zoezi la utoaji wa huduma za matibabu bure ( Afya check) jumamosi ya Septemba 9,2022.

Dkt Kimaro amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha huduma za afya Nchini hususan katika Hospitali hiyo ambapo mbali na ununuzi wa mashine hiyo , vifaa vingine vitakavyotumika kwenye chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum(ICU) pia vitanunuliwa.

"Wananchi wa Temeke wajiandae kupata huduma zilizo bora zaidi kutokana na msimamo na ufuatiliaji wa Serikali yao pendwa ya awamu hii ya Sita". Alisema

Akizungumza katika uzinduzi huo,muwakilishi wa mkuu wa wilaya ya Temeke ndugu Saadat Mtwale alisema zoezi hilo la utoaji huduma za afya bure kwa siku hizo tatu litakuwa mkombozi kwa Wananchi hasa wakazi wa Temeke kwa sababu baadhi yao hushindwa kupata huduma hizo kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama.

Bwana Hiyari Lubai mkazi wa Temeke amewashukuru wadau mbalimbali waliowezesha kufanikisha zoezi hilo huku akitoa wito kwa Wananchi kujitokeza kwa wingi kupata huduma hiyo.

# VIFAA TIBA VYA KIDIGITALI KUNUFAISHA WANANCHI WA TEMEKE.



Na **Sweetbetter Njige TMC Habari.** Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Jokate Mwegelo amezindua vifaa tiba vya kidigitali katika kituo cha afya Yombo Vituka kilichopo Manispaa ya Temeke.

Vifaa vilivyozinduliwa leo Agosti 17,2022ni 'Ultra sound' na 'X-ray' aina ya 'flat pannel detector digitalization' vyenye thamani ya sh .Mil 76 ikiwa ni pamoja na gharama za kufungwa kwake.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa vifaa hivyo Mhe.Jokate amewasisitiza watoa huduma wa Kituo hicho kuhakikisha wanatunza vifaa hivyo pia kutoa huduma bora kwa Wananchi na kuwapa kipaumbele Wazee wanapokuja kupata huduma.

"Nimpongeze Mhe.Rais kwa kuendelea kuwahudumia Wananchi katika sekta ya afya husani wakazi wa Temeke,tumepata zaidi ya bilioni 2 kwa ajili ya upanuzi wa hospitali ya Rangitatu,na leo tena vifaa tiba hivi vya milioni 76,tumshukuru sana mama Samia S uluhu Hassan".Alisema mkuu huyo wa Wilaya.

Kwa upande wake mganga mfawidhi wa kituo hicho Dkt. Boniface Mruma ameeleza matarajio yao baada ya ununuzi wa vifaa hivyo ikiwa ni pamoja na kuongeza utoaji wa huduma za kisasa kama vile upimaji wa ujauzito, kifua, moyo, mishipa ya damu , figo, uvimbe kwenye mfumo wa uzazi na kupunguza gharama za uendeshaji wa matibabu hayo.

Akizungumza wakati akimkaribisha mkuu wa Wilaya,Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya aliwataka watumishi kuendelea kutoa huduma bora na kutunza vifaa hivyo vilivyonunua kwa fedha za walipa kodi.

# MKURUGENZI TEMEKE AFURAHISHWA NA UTENDAJI KAZI WA WATUMISHI KITUO CHA AFYA YOMBO VITUKA.



Na **Jackson Wilson**
**TMC Habari.**

Ule usemi wa jitihada zinalipa umedhihirika kwa watumishi wa kituo cha afya Yombo Vituka,pale Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya alipotoa kiasi cha shilingi milioni 1 kuwapa motisha watumishi hao.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa mashine za kisasa za kidigitali za 'X-ray' na 'Utrasound' uliofanywa na mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe. Jokate Mwegelo Agosti 17,2022;Mabelya alisema kuwa watumishi katika Kituo hicho wamekuwa wakifanya kazi kwa kujituma.

"Mmekuwa mkifanya kazi vizuri na kwa kuwapa motisha ofisi yangu itatoa kiasi cha shilingi milioni moja,endeleeni kufanya kazi kwa bidii ili kumuunga mkono Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan".Alisema Mabelya

Katika kumuunga mkono Mkurugenzi huyo,mkuu wa wilaya Jokate aliahidi kutoa kiasi cha shilingi milioni 2 kuendelea kuwapa motisha watumishi hao ambapo awali aliwapongeza kwa kuweka safi mazingira ya Kituo hicho.

Motisha waliotoa Viongozi hao ni chachu kwa watumishi wengine katika sekta mbalimbali Nchini kufanya kazi kwa bidii na kujituma ili kulileta Taifa maendeleo.

Jarida hili limeandaliwa na;

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**MANISPAA YA TEMEKE**

***www.temekemc.go.tz***